



Centrepay

Mtu wa 1: Je, ulijua kuwa Services Australia ina huduma ya bure ya kukusaidia kudhibiti na kulipia bili zako?

Mtu wa 2: Hapana, inaitwaje na inafanya kazi zipi?

Mtu wa 1: Inaitwa Centrepay. Ni huduma ya kulipia bili kwa bure na hiari. Unaweza kuchagua kupata kiasi kidogo cha pesa kukatwa kutoka kwa malipo yako ya Centrelink kila wiki mbili ili kulipa bili zako.

Mtu wa 2: Je, Centrepay inawezaje kunisaidia?

Mtu wa 1: Centrepay ni njia nzuri kudhibiti na kulipa gharama yako ya ukaya ya kila mara, kama:

- kodi
- simu
- umeme, gesi na maji
- huduma za matibabu
- ada za utunzaji wa watoto
- ada za shule, na bili nyingi nyingine.

Centrepay hukusaidia kulipa bili zako kwa wakati. Unachagua:

- bili za kulipia kupita Centrepay
- kiasi gani cha kukatwa kutoka kwa malipo yako ya Centrelink kila wiki mbili.

Kiasi cha chini kabisa unaweza kukatwa ni \$10 kwa wiki mbili.

Unaweza kutumia Centrepay tu kwa bidhaa na huduma zinazotolewa na biashara zilizoidhinishwa.

Mtu wa 2: Je, nitapataje biashara iliyoidhinishwa?

Mtu wa 1: Unaweza kutumia kifaa cha utafutaji cha **kupata biashara au shirika** kwenye tovuti kutafuta kwa biashara katika eneo lako. Kinaorodhesha biashara zinazoidhinishwa kutumia Centrepay.

Ikiwa biashara au mtu ambaye unataka kulipa hayupo kwenye orodha, wasiliana nao. Waulize ikiwa wanakubali kupokea malipo kwa kutumia Centrepay. Wasipofanya hivyo, waambie wafikirie kujiunga.

Mtu wa 2: Je, ninawezaje kuweka makato ya Centrepay?

Mtu wa 1: Unaweza kuanza, kubadilisha, kukagua au kusimamisha kukatwa kwa Centrepay wakati wowote kwa:

- kuomba biashara unayotaka kulipa, kuanzisha kwa ajili yako
- kutumia akaunti yako ya Centrelink mtandaoni kupita myGov

- kutumia programu ya Express Plus Centrelink kwenye kifaa chako cha mkononi
- kutembelea kituo cha huduma
- kutupigia simu kwenye **131 202** kuzungumza na mtu katika lugha yako.

Mtu wa 2: Je, ninaweza kupata wapi maelezo zaidi kuhusu Centrepay?

Mtu wa 1: Unaweza kujua zaidi katika Kiingereza kwenye **servicesaustralia.gov.au/centrepay** au piga simu kwa **131 202** ili kuzungumza na mtu katika lugha yako. Nambari ile ya simu tena ni – **131 202**.

Gharama za kupiga simu zinaweza kutofautiana kulingana na mtoa huduma wa simu. Kunaweza kuwa na malipo ya juu zaidi ya simu kutoka kwa simu za umma na simu za mkononi.

Kanusho

Taarifa iliyo katika chapisho hili inakusudiwa tu kama mwongozo wa malipo na huduma. Ni wajibu wako kuamua kama ungependa kutuma maombi ya malipo na kutuma maombi kuhusiana na hali yako mahususi.



Centrepay

Person 1: Did you know Services Australia has a free service to help you manage and pay your bills?

Person 2: No, what is it called and how does it work?

Person 1: It is called Centrepay. It is a free and voluntary bill paying service. You can choose to have small amounts of money deducted from your Centrelink payments each fortnight to pay your bills.

Person 2: How can Centrepay help me?

Person 1: Centrepay is a great way to manage and pay your regular household expenses, like:

- rent
- telephone
- electricity, gas and water
- medical services
- child care fees
- school fees, and many other bills.

Centrepay helps you pay your bills on time. You decide:

- the bills to pay through Centrepay
- how much to deduct from your Centrelink payments each fortnight.

The lowest amount you can deduct is \$10 per fortnight.

You can only use Centrepay for goods and services provided by approved businesses.

Person 2: How do I find an approved business?

Person 1: You can use the **find a business or organisation** search tool on our website to search for businesses in your area. It lists businesses approved to use Centrepay.

If a business or person you want to pay is not on the list, contact them. Ask them if they accept payments using Centrepay. If they do not, ask them to consider joining.

Person 2: How do I set up a Centrepay deduction?

Person 1: You can start, change, check or stop a Centrepay deduction at any time by:

- asking the business you want to pay, to set it up for you
- using your Centrelink online account through myGov
- using the Express Plus Centrelink app on your mobile device
- visiting a service centre
- calling us on **131 202** to speak to someone in your language.

Person 2: Where can I find out more about Centrepay?

Person 1: You can find out more in English at servicesaustralia.gov.au/centrepay or call **131 202** to speak to someone in your language. That number again – **131 202**.

Call charges may vary depending on the telephone service provider. There may be higher call charges from public telephones and mobile phones.

Disclaimer

The information contained in this publication is intended only as a guide to payments and services. It's your responsibility to decide if you wish to apply for a payment and to make an application with regard to your particular circumstances.